

UNIVERSITY OF NAIROBI

CHUO KIKUU CHA NAIROBI TUWE MFANO BORA by Dr. Arthur Kemoli

Chuo Kikuu cha Nairobi  
Kwa mwito wetu wa umoja kazini  
Chuo Kikuu cha Nairobi  
Sote tufanye kazi bila ufisadi.

Kufagia pembeni kote kwa Chuo Kikuu  
Wanafunzi, Wafanyi kazi na walimu  
Uzambe tuache, midhamu tuweke Chuo Kikuu  
Oh Kweli  
Chuo Kikuu cha Nairobi  
Sote tufanye kazi bila ufisadi.

2. Tuwe kielelezo  
Kwa elimu na kutafuta ukweli  
Basi panapo ukweli  
Udanganyifu, hongo, rushwi hazikai

Kupandishwa cheo, na haki ifanywe ionekane  
Mali ya umma, tutie mkazo tulinde vyeema  
Oh kweli  
Basi Panapo ukweli  
Udanganyifu, hongo, rushwa hazikai

3. Tu Chemi Chemi ya elimu  
Na kwa maono tuna mwangaza mbele  
Chuo Kikuu Cha Nairobi  
Tujiheshimu na Kenya ituheshimu

Kwa mitihani usingoje kutoa hongo  
Na mwalimu isukubali kupewa hongo  
Usionyesha mapendeleo kwa mitihani  
Oh kweli  
Chuo Kikuu Cha Nairobi  
Tujiheshimu na Kenya ituheshimu.

4. Chuo Kikuu Cha Nairobi  
Kwa mwito wetu wa umoja kazini  
Tutafagia ufisadi  
Kwa kila pembe ya chuo kikuu chetu

Chuo Kikuu twasonga mbele, twasonga mbele  
Mfano bora kwa Kenya nzima, kwa Kenya nzima

Oh! Kweli

Tutafagia ufisadi  
Kwa kila pembe ya Chuo Kikuu chetu.